JARIDA TOLEO LA APRILI - JUNI 2022

# FAHARI YETU
## HALMASHAURI YA ARUSHA

Arusha Dc Kazi Inaendelea



# Milioni 740 Upanuzi wa Zahanati ya Mwandeti kuwa Kituo cha Afya



# TAHARIRI

Karibu msomaji wa Jarida La FAHARI YETU halmashauri ya Arusha toleo la Mwezi Aprili - Juni 2022, Jarida linalomilikiwa na Halmashauri ya Arusha na hutolewa kila baada ya miezi mitatu.

Dhima ya Jarida hili ni kutoa habari kwa Umma juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Serikali kupitia Halmashauri ya Arusha kwa kipindi cha miezi mitatu ili kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa wananchi na kuwa daraja la utawala bora, kadhalika ni nyenzo ya kukuza Maarifa na Maendeleo katika halmashauri ya Arusha.

Malengo mahususi ya Jarida hili ni kuhakikisha wananchi wanapata habari na taarifa kwa wakati, namna ambavyo halmashauri yao, inafanya kazi na kutekeleza jukumu lake la kuwahudumia wananchi kisekta.

Aidha tunaendela kutoa habari na makala mbalimbali kupitia kurasa za mitandao ya kijamii za halmashauri,ili kuwafikia wananchi kwa makundi na kuuhabarisha Umma namna Sera zinavyotungwa, Mipango inavyopangwa na utekelezaji wake.

Matoleo ya Jarida la FAHARI YETU yatasheheni taarifa na makala zenye kuhabarisha, kuelimisha kuhamasisha, kuburudisha na kuchochea maendeleo ya mtu mmoja mmoja, kaya na jamii kwa ujumla wake.

Hata hivyo tunakaribisha habari kutoka kwenye Vitongoji, Vijiji na Kata ambazo zinaweza kueleza jinsi shughuli mbalimbali zinazofanyika kwenye maeneo hayo kisekta pamoja na Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa.

Kadhalika tunakaribisha maoni na ushauri wa kuboresha Jarida la FAHARI YETU ili kuweza kutimiza malengo ya halmashauri ya Arusha ya kufanya kazi kwa uwazi, ukweli na hakika, pamoja na uwajibikaji wenye tija.

Tunakutakia usomaji mwema wa Jarida lako la FAHARI YETU Halmashauri ya Arusha.



**MHE. OJUNG'U PINIEL SALEKWA**
**MWENYEKITI HALMASHAURI YA ARUSHA**



**SELEMAN HAMIS MSUMI**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA ARUSHA**

# YALIYOMO

01 Serikali yatoa Milioni 740 Upanuzi Zahanati ya Mwandeti kuwa Kituo cha Afya
02 Milioni 400 za mapato ya ndani zajenga kituo kipya cha Afya Oloirieni
03 Milioni 470 za SEQUIP zajenga shule ya sekondari kata ya Kiutu
04 Wananchi wa Mwandet kuondokana na adha ya Maji
05 Serikali yatoa milioni 500 upanuzi kituo cha Afya Oldonyosambu
06 Mradi wa binti na Maendeleo waleta Mapinduzi Musa, waepusha Wasichana na Ndoa za Utotoni
07 Milioni 90 za Tozo zajenga nyumba ya Watumishi Kituo cha Afya Mwandeti
08 TASAF yawezesha ujenzi wa Kivuko Moivo, huku walengwa wakinufaika na ajira za Muda
09 Jamii yaaswa kutofumbia macho vitendo vya Ukatili dhidi ya Watoto
10 Waathirika wa VVU washauriwa kuachana na Imani potofu badala yake kuendelea kutumia ARVs
11 Walimu waagizwa kusimamia kila Mwanafunzi kuotesha mti na kuutunza wawapo Shuleni
12 Wafadhili waahidi kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika Sekta ya Elimu
13 Walimu wahimizwa kuzingatia kujisomea kupitia programu ya MEWAKA
14 Baada ya Bweni la Wasichana, TASAF yawakumbuka wavulana Sekondari Oldonyowas
15 Mkurugenzi wa OPEC FUND aridhishwa na utekelezaji wa Miradi ya TASAF Nchini
16 Vikundi vya walengwa wa TASAF vyaanza Kuimarisha Uchumi wa Kaya
17 Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Arusha 2022
18 Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa amewataka vijana kutumia fursa ya Mikopo isiyo na riba inayotolewa na Halmashauri
19 Mwenyekiti Arusha DC aitaka jamii kuwahudumia wajawazito
20 Serikali yakabidhi Pikipiki 48 kwa Maafisa Kilimo Halmashauri ya Arusha
21 Mradi wa BOOST watua Arusha DC
22 RC Mongela aongoza wafanyakazi Mkoa wa Arusha Sherehe za Mei Mosi 2022
23 TEA yaondoa Msongamano wa wanafunzi madarasani Sekondari ya Sokoni II
24 Wafugaji Watakiwa kutumia majosho kuogeshea Mifugo kwa Ufugaji wenye tija
25 Serikali Yakumbuka Vituo vya Walimu - (TRC) ARUSHA DC
26 Wanufaika wa TASAF wamshukuru mama Samia
27 Shiriki Sensa ya watu na Makazi



Maendeleo ya upanuzi wa Zahanati ya Mwaneti kuwa Kituo cha Afya

# SERIKALI YATOA MILIONI 740 UPANUZI ZAHANATI YA MWANDETI KUWA KITUO CHA AFYA

**Na Elinipa Lupembe**

Serikali ya awamu ya sita imeendelea kuboresha huduma za afya nchini, huku halmashauri ya Arusha ikiwa ni miongoni mwake, kwa kusogeza huduma za afya karibu na wananchi hususani maeneo ya vijijini, lengo likiwa ni kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya sambamba na kupunguza vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua.

Katika kutimiza adhma hiyo, Serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi milioni 740 kwa ajili ya upanuzi wa zahanati ya Mwandeti, ili kukipa hadhi kuwa Kituo cha afya, kiweze kutoa huduma nyingi zaidi tofauti na ilivyokuwa hapo awali ikiwa ni zahanati.

Akizungumza na mwandishi wetu, Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, amebainisha kuwa, halmashauri imepokea kiasi hicho cha fedha, kwa awamu tatu tofauti, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika zahanati hiyo ili kuwa hadhi ya Kituo cha Afya.

Amesema kuwa fedha hizo zimetumika kujenga jengo la wagonjwa wa nje 'OPD', jengo pacha la mama na mtoto likiwa na jengo la upasuaji (theater & maternity ward), Maabara, sehemu ya kuchomea taka pamoja na nyumba moja ya watumishi yenye uwezo wa kuishi Familia tatu (3 in 1).

"Ninaipongeza Serikali ya awamu ya sita, inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuwakumbuka na kuwahurumia kina mama wajawazito na watoto, waliokuwa wakihatarisha maisha na wengine kupoteza maisha wakati wa kujifungua, kutokana na kukosa huduma za haraka wakati wa kujifungua, uwepo wa Kituo hicho utapunguza ama kuondoa kabisa vifo visivyo vya lazima." Amesisitiza Mkurugenzi Msumi.

Aidha Msumi ametaja mchanganguo wa milioni 740, kulingana na vyanzo vyake kuwa milioni 150 fedha kutoka serikali Kuu, milioni 500 fedha za tozo ya miamala ya simu, na milioni 90 fedh za mapambano dhidi ya UVIKO 19.

Naye Mganga Mfawidhi, Zahanati ya Mwandeti, Dkt. Aidan Martin, amesema uwepo wa kituo cha afya Mwandeti, utasaidia upatikanaji wa huduma muhimu ambazo hazikupatikana hapo awali kwenye zahanati, huku wagonjwa wakilazimika kwenda hosptiali ya wilaya ya Olturumeti umbali wa zaidi ya Kilomita 35, jambo lililoongeza gharama na kuhatarisha maisha ya wagonjwa.

"Tulikuwa tunatoa rufaa nyingi kwa wagonjwa, lakini uwepo wa kituo cha afya, tunatarajia huduma nyingi zitapatikana hapa na kutakuwa na oingezeko la wagonjwa kutoka wastani wa wagonjwa 1,200 mpaka 1,700 kwa mwezi." Ameweka wazi Daktari Aidan.

Hata hivyo wananchi wa kata ya Mwandeti husasani kijiji cha Engalaoni, ambao hutumia zahanati ya Mwandeti kwa matibabu, wameishukuru Serikali kwa kuona umuhimu kwa kuwapa fedha za kuongeza miundo mbinu ya majengo, ili zahanati hiyo ipandishwe hadhi na kuwa kituo cha afya jambo ambalo wamethibitisha kuwa Mungu amewaonekania kwa kusikia kilio chao.




Diwani wa kata ya Mwandeti, Mhe. Logolie Lukumay amethibitisha kuwepo kwa changamoto za matibabu kwa wagonjwa wa kijiji cha Engalaoni, hasa kwa kuzingatia kijiji hicho kiko mwishoni mwa kata na wilaya pia.

Ameongeza kuwa, kuwepo kwa Kituo cha afya, licha ya wananchi kuwa na uhakika wa kupata matibabu, lakini pia kitapunguza gharama za usafiri kufuata matibabu na zaidi, itasaidia kupunguza vifo visivyo vya lazima hasa kwa kina mama wajawazito wanaohitaji kufanyiwa upasuaji pamoja na watoto wanaozaliwa.

"Tunaishukuru Serikali ya awamu ya sita, tunamshukuru sana Mama Samia ametufuta machozi ya muda mrefu, zahanati hii inahudumia watu wa Engalaoni na kata jirani za wilaya ya Monduli, watu waliteseka sana kutafuta matibabu, kina mama wajawazito wanapohitajika kufanyiwa 'operation' ilikiwa ni shida, hata kupata usafiri wa kufika hospitali ya wilaya ni changamoto kutoakan na umbali." Amefafanua Mheshimiwa Logolie.

Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya Zahanati ya Mwandeti, kunategemea kukipandishwa hadhi na kuwa kituo cha afya, kituo ambacho kitahudumiza zaidi ya watu elfu 15 wa kata ya Mwandeti na kata ya jirani ya Mferejini, wilaya ya Monduli.








Muonekano wa kituo kipya cha Afya Oloirieni

# MILIONI 400 ZA MAPATO YA NDANI ZAJENGA KITUO KIPYA CHA AFYA OLOIRIENI

Na Elinipa Lupembe

Halmashauri ya Arusha, imetekeleza mradi wa ujenzi wa Kituo kipya cha afya kata ya Oloirieni, kwa gharama ya shilingi milioni 450, huku milioni 400 zikiwa ni fedha za mapato ya ndani ya halmashauri hiyo kupitia fidia ya deni la Lakilaki huku milioni 50 zikiwa ni fedha kutoka Serikali Kuu.

Mradi huo umetekelezwa kwenye kata hiyo, kukiwa na uhitaji mkubwa wa huduma hiyo ya afya, kutokana na idadi kubwa ya watu katika eneo hilo na upatikanaji wa huduma za afya kwenye hospitali ya serikali kuwa mbali, jambo linalosababisha wagonjwa kutibiwa kwenye hospitali za binafsi, na kuwafanya wananchi kutumia gharama kubwa kupata matibabu huku wengine wakishindwa kumudu gharama hizo.

Hata hivyo wananchi wa kata ya Oloirien, wameishukuru serikali yao ya awamu ya sita, inayoongozwa na Mama Samia Suluhu, kupitia uongozi wa halmashauri, kwa kuwapelekea miradi ya zaidi ya shilingi milioni 650 kwa kipindi kifupi, miradi ambayo wamekiri haijawahi kutokea hapo awali.

"Tunaishukuru sana serikali ya awamu ya sita, kata ya Oloirieni haijawahi kupata miradi mikubwa yenye fedha nyingi kwa wakati mmoja, ndani ya miezi sita tumepata fedha kiasi cha shilingi milioni 650 za kutekeleza miradi mikubwa miwili, hii haijawahi kutokea tangu kata hii imenazishwa" wameshuhudia wananchi hao.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Oloirieni, mheshimiwa John Aminiel, ameishukuru serikali pia kwa mradi wa kituo cha afya, na kusema kuwa wananchi wa kitongoji chake wameamua kutoa kipande cha ardhi chenye ukubwa wa mita 20, ili kuongeza ukubwa wa eneo la kituo hicho kwa ajili ya kujenga majengo ya wodi za wagonjwa ili kituo hicho kukidhi sifa za nyota tano.

Naye Afisa Mtendaji kata ya Oloirien, Charles Sikoi amesema kuwa kiasi hicho cha fedha kitahusisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), ujenzi wa jengo pacha la mama na mtoto na upasuaji (martenity ward & theater), ujenzi wa maabara pamoja na kichomea taka na kuongeza kuwa kituo hicho kinategemea kuhudumia watu elfu 14 wa kata hiyo na kata za jirani .

Awali halmashauri ya Arusha, imeendelea kutekeleza mkakati wa serikali wa kusogeza huduma za afya karibu na wananchi na kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ndani ya eneo lake ili kufikia lengo la kitaifa la kutokomeza vifo vya mama wajawazito na watoto wakati wa kujifungua.





Jengo la ghorofa 2 lenye vyumba 8 vya madarasa, maktaba & maabara ya TEHAMA.

# MILIONI 470 ZA SEQUIP ZAJENGA SHULE YA SEKONDARI KATA YA KIUTU.

Na Elinipa Lupembe

Serikali kupitia Wizara ya Elimu imeto fedha shilingi milioni 470, ikiwa ni fedha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (SEQUIP), kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika kata ya Kiutu.

Ujenzi huo wa sekondari mpya, unaendelea kwa kasi, huku wananchi wa kata hiyo wakijitoa kwa hali na mali kufanyakazi mbalimbali katika eneo hilo, ili kuharakisha ukamilishaji wa ujenzi ili watoto wao waweze kuanza kusoma shuleni hapo mapema Januari 2023.

Wananchi wa Kata hiyo ya Kiutu na vitongoji vyake wamekiri kufurahishwa na ujenzi wa shule hiyo katika kata yao na kujitolea kufanya kazi za mikono kuharakisha ujenzi huku wakimpongeza na kumshukuru mheshimiwa Rais Mama Samia, kwa kuwajali wao na watoto wao.

"Mama ameupiga mwingi, sisi wanakiutu tumeshuhudia kwa maneno na vitendo, kata yetu haijawahi kuwa na shule ya sekondari, watoto wetu husoma kata za jirani, kila mwaka tunachangia maendeleo ya shule za kata nyingine, imefika wakati sasa, na sisi tunachangia maendeleo ndani ya kata yetu". Wamesisitiza wananchi wa kata ya Kiutu.

Afisa Elimu Sekondari, Mwl. Menard Lupenza amesema kuwa, fedha hizo, milioni 470 zinatumika katika ujenzi wa jengo la utawala, jengo la ghorofa mbili lenye vyumba 8 vya madarasa, maktaba, maabara ya somo la TEHAMA na matundu ya vyoo, na majengo mengine mawaili yenye maabara za masomo ya Sayansi Kemia, Fizikia na Baiolojia.

"Niseme tu kwamba, ujenzi wa shule hii, unategemea kukamilika mapema, huku taratibu nyingine za usajili wa shule zikiendelea, na kuhakikisha ifikapo Januari 2023, anafunzi wa kidato cha kwanza kuanza kusoma shuleni hapa" amesisitiza Afisa Elimu Lupenza.

Ikumbukwe kuwa kata ya Kiutu ni miongoni mwa kata ambazo hazikuwa na shule ya sekondari, baada ya serikali kutoa fedha wananchi watatu wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Kiutu Mhe. Malaki Malambo walijitoleo eneo lenye ukubwa wa Mita za mraba 11,777.2, kwa ajili ya ujenzi wa shule hilo.

Baada ya kukamilika kwa ujenzi wa sekondari Kiutu, halmashauri ya Arusha itakuwa na jumla ya shule 37 za serikali na shule 23 za binafsi, na kufanya halmasahuri kuwa na jumla ya shule 57 za Sekondari.





# WANANCHI WA MWANDET KUONDOKANA NA ADHA YA MAJI

Na Elinipa Lupembe

Wananchi wa kata ya Mwandeti, wanategemea kuondokana na adha ya kukosekana kwa uhakika wa maji safi na salama, kufuatia Serikali kuanza utekelezaji wa mradi wa maji wa vijiji vitano, unaojulikana kama Losikito – Mwandet, kwa gharama ya shilingi bilioni 2.5 fedha za serikali Kuu kupitia Mfuko wa Maji.

Wananchi hao wamethibitisha kukabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa uhakika wa maji safi na salama katika eneo lao, kutokana na vijiji hivyo kutokuwa na miundombinu ya uhakika ya maji kwa kipindi kirefu sasa.

Wakizungumza na mwandishi wetu alipotembelea eneo la Mradi, wameweka wazi kuwa, changamoto ya kukosekana kwa maji, katika eneo lao inarudisha nyuma maendeleo ya familia zao kiuchumi na hata kijamii, kwa kuwa wanatumia muda na gharama kubwa kutafuta maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, badala ya kufanya shughuli nyingine za kifamilia na uzalishaji.

Witnes Joel, mkazi wa Losikito amebainisha kuwa, wanawake wanateseka kutafuta maji, wakati mwingine hutembea na punda kwenda kuchota maji, maeneo ya mbali na wakati mwingine hufika mpaka maeneo ya Ngaramtoni umbali wa zaidi ya Km 20 na kununua maji kwa shilingi elfu 3 kwa dumu la lita 20.

Naye Ngaremu Laban (69), ameipongeza serikali kwa kutekeleza Mradi wa maji katika kata yao na kuahidi kuutunza mradi huo, huku akiwasihi wanawake wenzie kuutunza na kuuthamini mradi huo pindi utakapokamilika kwa kuwa utawasaidia wananchi wote hususani wanawake ambao ndio wahanga wakubwa pindi maji yanapokosekana.

Mradi huu wa maji utahudumia wananchi 11, 118 wa vijiji vitano vya kata ya Mwandet, mradi unaotegemewa kutatua changamoto ya ukosefu wa maji ya uhakika inayowakabili wananchi wa eneo hilo.








Dkt. Alkhalifa Abdulhamid Saleh, Mkurugenzi wa Umoja wa Nchi zinazozalisha Mafuta kwa wingi Duniani (Opec Fund)

# SERIKALI YATOA MILIONI 500 UPANUZI WA KITUO CHA AFYA OLDONYOSAMBU.

Na Elinipa Lupembe;

Kufuatia mkakati wa serikali wa kuboresha miundombinu ya vituo vya kutolea huduma ya afya, wananchi wa kata ya Oldonyosambu, halmashauri ya Arusha wameendelea kuneemeka kwa kupatiwa mradi wa upanuzi wa kituo afya Oldonyosambu.

Akizungumza wakati wa kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, amefafanua kuwa halamsahuri imepokea fedha kwa awamu mbili, awamu ya kwanza shilingi milioni 300 fedha kutoka Serikali Kuu na awamu pili milioni 200 fedha kupitia miradi ya Lipa kwa na Matokeo 'Result Based Financing' na kufanya jumla ya shilingi milioni 500.

Aidha Mkurugenzi Msumi ameongeza kuwa, mradi huo ni muhimu kwa wananchi wa Oldonyosambu, kwa kuzingatia malengo ya serikali ya awamu ya sita, ya kuboresha huduma za afya kwa kusogeza huduma hizo muhimu, karibu na wanachi, kwa kuhakikisha kila kata inakuwa na kituo cha afya chenye hadhi ya nyota tano, huku kila kijiji kikiwa na Zahanati.

Mkuu wa Idara ya Mipango halmashauri hiyo, Anna Urio, amefafanua kuwa kiasi hicho cha shilingi milioni 500, kitahusisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo pacha litakalojumuisha wodi ya mama na mtoto (maternity ward), sehemu ya kujifungulia (labour word) na sehemu ya upasuaji (theater), Jengo la huduma ya chanjo kwa mama na mtoto (RCH), jengo la Maabara, jengo la Mionzi (X-ray), jengo la kufulia pamoja na nyumba ya Watumishi , lengo likiwa ni kuongeza majengo muhimu ya kutolea huduma zote za Afya katika kituo hicho.



Naye Mganga Mfawidhi Kituo cha Afya Oldonyosambu, Dkt. Aziza Said, amezungumzia umuhimu wa upanuzi wa kituo hicho cha afya, kutokana na uhitaji mkubwa wa huduma za upasuaji hasa kwa kina mama wajawazito.

"Kuna uhitaji mkubwa wahuduma za upasuaji hasa kwa wajawazito kwa kuwa, mara nyingi tunawapa rufaa kwenda hospitali ya wilaya ya Olturumet, jambo ambalo huhatarisha maisha, uwepo wa huduma zote utasaidia kuokoa maisha na hata kupunguza gharama kwa wagonjwa" .Amefafanua Dkt. Aziza.

Ukamilishaji wa kituo hicho cha afya utafanya halmashauri ya Arusha kuwa na jumla ya vituo 6 vya afya vinavyomilikiwa na serikali na vituo 2 vya binafsi.

# MRADI WA BINTI NA MAENDELEO WALETA MAPINDUZI MUSA, WAEPUSHA WASICHANA NA NDOA ZA UTOTONI









Na Elinipa Lupembe

Mradi wa Binti na Maendeleo unaotekelezwa na Shirika la DSW Tanzania, umefanikiwa kuzuia ndoa za utotoni kwa wasichana waliokuwa wamechumbiwa tayari kuolewa, kwa kuwafanya wasichana hao, kukataa kukatisha masomo yao na kuolewa badala yake kuendelea na masomo yao, mradi unatekelezwa kupitia vikundi vya uelimishaji rika pamoja na klabu za wapinga ukatili ndani ya shule za msingi.

Inaendelea Uk.7

*Inatoka Ukurasa wa 6*

Hayo yamewekwa wazi wakati wa mdahalo, uliohusisha wawakilishi kutoka makundi mbalimbali ya kijamii, wakati wa Bonanza maalum la Binti na Maendeleo, liliofanyika kwenye viwanja vya shule ya Msingi Musa kata ya Musa, halmashauri ya Arusha, Bonanza lenye lengo la kupaza sauti ya kuelimisha jamii juu ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Mdahalo huo, kwa pamoja wameupongeza Mradi wa Binti na Maendeleo, mradi ambao wamethibitisha kuleta mapinduzi makubwa kwa kuwajengea uwezo wa kufahamu na kutambua, uhalisia wa suala zima la ukatili wa kijinsia, hususani ukeketaji na ndoa za utotoni pamoja na madhara yake, ukatili ambao ulikuwa ukifanyika katika maeneo hayo kutokana na mila na desturi za kabila la kimaasai, ambazo wanadai wao wamerithi kutoka kwa mababu zao.

"Kupitia elimu inayotolewa na vijana waelimisha rika walio nje ya mfumo rasmi wa elimu, na klabu za watoto shule ya msingi Olchoruvus, jamii yetu ya Musa sasa imepata kufahamu madhara ya ukeketaji na kuanza kuachana na mila hiyo na zaidi jamii imetambua umuhimu wa kuwasomesha watoto wa kike, watoto ambao hapo awali walikatishwa masomo na wazazi wao na kulazimika kuolewa katika umri mdogo" wamesisitiza Wanajamii ya Musa.

Hosiana Rafael mwanafunzi wa shule ya msingi Olchorovus, amebainisha kuwa, kupitia klabu yao ya Binti na Maendeleo shuleni, imefa - nikiwa kuwaelimisha wanafunzi wenzao kupinga na kupambana ukeketaji pamoja na ndoa za utotoni na kuongeza kuwa, elimu hiyo imefanikisha baadhi ya wasichana waliochumbiwa wameweza kuzungumza na wazazi wao na kukataa kuolewa na kuamua kuendelea na masomo yao na wazazi wao wamewakubalia.

"Tunashukuru kwa sasa wazazi wetu wameanza kutuelewa, wengi wameanza kutambua madhara ya ukeketaji, na wazazi wengi sasa wameacha kuwaozesha watoto wao wakiwa shule na kuamua kuwaacha waendelee na masomo, na mpaka sasa wasichana hao wapo shuleni, DSW imetuletea ukombozi hasa kwa wasichana wa kata ya Musa" ameweka wazi mwanafunzi Hosiana

Mgeni rasmi katika Bonaza hilo, Afisa Maendelo ya Jamii, Ofisi ya Mkuu wa mkoa Arusha Erena Materu, licha ya kulishukuru shirika la DSW kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa jamii, amewapongeza kwa kuungana na Serikali kupambana na ukatili wa kijinsia hususani kwa wanawake na watoto, kazi ambayo ni mkakati wa Serikali ya awamu ya sita sambamba na utekelezaji wa Ilani ya CCM 2021/2025.

Aidha ameipongeza jamii ya watu wa Musa kwa kupokea na kuyatumia maarifa waliyopata na kuwataka kutumia maarifa hayo, kuendelea kuelimishana wao kwa wao, ili jamii nzima ipate uelewa wa pamoja wa kutokomeza mila potofu, mila ambazo zina madhara makubwa kisaikolojia, kijamii na kiuchumi, na kusisitiza kuwa Arusha bila Ukatili inawezekana.

"Haya mambo mazuri tuliyofundishwa na DSW, tuyaendeleze na kuyafanyia kazi kwa kuelemisha wenzetu kwa nguvu moja, tukiungana kwa pamoja kupinga ukatili katika jamii zetu, viongozi wa mila na dini wakisema, viongozi wa Serikali na wale vyama vya siasa nao wakisema, baba na mama wakisema, vijana wa kike na wakiume wakisema, watoto wakisema, ninaamini ukeketaji na ndoa za utotoni vitakwisha na kubaki na jamii huru yenye maamuzi sahihi kwa maendeleo ya taifa letu" amesisitiza Erena.

Mratibu wa Mradi wa Binti na Maendeleo shirika la DWS Tanzania, Juliana Mndanga, ameeleza lengo la Bonanza hilo ni kuwakutanisha pamoja, watu wa makundi na mitazamo tofauti, ili kuelemisha na kuwahamasisha kupinga ukatili wa kijinsia kwa sauti moja, kupitia shughuli za kijamii ikiwemo burudani za sanaa za ngoma na nyimbo, michezo, jumbe mbalimbali pamoja na midahalo.

"Kupitia Bonanza hili jamii imeweza kufahamu kuwa jamii yao, inakabiliwa na changamoto ya ukatili wa kijinsia, ukeketaji na ndoa za utotoni, kupitia shughuli mbalimbali zinazofanyika kwenye Bonanza, zinawezesha kutambua madhara ya matukio hayo ya ukatili na namna ya kuyapinga na kuyatokomeza kabisa, huku jamii ikitakiwa kutambua kuwa wakiwapa nafasi wasichana wanawaweza" amesisitiza Juliana.

Hata hivyo Mratibu huyo wa mradi ameweka wazi kuwa, DSW kwa kushirikiana na halmashauri ya Arusha inatekeleza Mradi wa Binti na Maendeleo kwenye shule za msingi ndani ya kata tano za Musa, Mwandet, Olmotony, Ng'iresi na Sokon II, huku kukiwa na klabu za kupinga ukatili shuleni na vijana waelimisha rika walio nje ya mfumo rasmi wa elimu.





Mwonekano wa sasa wa nyumba ya Watumishi, Kituo cha Afya Mwandet

# MILIONI 90 ZA TOZO ZAJENGA NYUMBA YA WATUMISHI KITUO CHA AFYA MWANDET

Serikali kupitia wizara ya Afya, inaendelea na mkakati wa kuboresha miundombinu ya huduma za afya, unaoenda sambamba na ujenzi wa nyumba za watumishi wa Afya, ili wahudumu kuwa na makazi katika maeneo yao ya kazi pamoja na kuhakikisha wananchi hasa wa maeneo ya pembezoni wanapata huduma za afya kwa masaa 24.

Kupitia mkakati huo, wakazi wa kata ya Mwandeti na vitongoji vyake wamepata neema hiyo ya kuongezewa miundombinu ya iliyokuwa zahanati ya Mwandeti na kuwa kituo cha afya, sambamba na ujenzi wa nyumba ya wahudumu wa afya.

Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi ameweka wazi kuwa, halmashauri yake, ilipokea kiasi cha shilingi milioni 90, kutoka Serikali kuu, ikiwa ni fedha za tozo za miamala ya simu, kwa ajili kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba ya watumishi wa kituo kipya cha afya Mwandeti, yenye sehemu ya kuishi watumishi watatu (3 in 1).

Aidha amefafanua kuwa, utekelezaji wa mradi huo, unaendelea vizuri, uko hatua za ukamilishaji, na unategemea kukamilika mwishoni mwa mwaka huu wa fedha, tayari kwa watumishi wa kituo hicho cha afya, kuanza kuishi na kuendelea na majukumu yao ya kuwahudumia wagonjwa, kama malengo ya Serikali yanavyoainisha.

"Niseme tu, Serikali ya awamu ya sita inatambua, kazi kubwa inayofanywa na wahudumu wa afya, inatambua mazingira yao ya kazi, ndio maana ina mkakati wa kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya, pamoja na mazingira rafiki ya kuishi watumishi wa afya, hususani maeneo ya pembezoni ambayo yanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa nyumba za kuishi" amefafanua Mkurugenzi Msumi.

Naye Mganga Mfawidhi Zahanati ya Mwandeti, Dkt. Aidan Martin amesema kuwa, ujenzi wa nyumba hizo za watumishi, umekuja kwa wakati sahihi kwa kuwa,

uwepo wa nyumba za watumishi katika eneo la kazi, utawaongezea ari ya kufanya kazi, itaongeza weledi katika kutekeleza majukumu yao, ikiwa ni pamoja na utoaji na upatikanaji wa huduma kwa wagonjwa kwa urahisi na kwa haraka wa muda wote wa siku.

"Daktari na wauguzi wanaposihi ndani ya eneo la kazi, inawarahisishia utekelezaji wa majukumu yao ya kazi, kuingia kazini kwa wakati, kutoa huduma kwa haraka hususani huduma za dharura hasa wakati wa usiku, lakini pia inaongeza wigo kwa wagonjwa kupata huduma kwa saa 24, kwa kuwa wauguzi wanapatikana eneo hilo kwa muda wote" amesema Dkt. Martin

Awali ujenzi wa nyumba hiyo ya watumsihi wa afya, umeenda samabamba na upanuzi wa miundombinu ya zahanati ya Mwandeti ili kuwa kituo cha afya, upanuzi uliohusisha ujenzi wa nyumba hiyo ya watumishi, jengo la wagonjwa wa nje, jengo la mama na mtoto, maabara, jengo la X-ray na Laundry kwa gharama ya shilingi milioni 500.





Wanufaika TASAF wakishiriki katika Ujenzi wa Kivuko Kijiji cha Moivo

# TASAF YAWEZESHA UJENZI WA KIVUKO MOIVO, HUKU WALENGWA WAKINUFAIKA NA AJIRA ZA MUDA.

Na Elinipa Lupembe

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF kupitia mradi wa mpango wa kunusuru kaya Masikini, unaendelea kuzinufaisha kaya hizo, kwa kutoa ajira za muda kupitia miradi iliyoibiliwa na kaya hizo na kutekelezwa katika maeneo yao.

Kijiji cha Moivo, kata ya Moivo ni miongoni mwa vijiji 88 vya halmasahauri ya Arusha, vinavyonufaika na mpango huo unaotekelezwa na TASAF awamu ya III, kikiwa na walengwa 250.

Akizungumza kwenye eneo la ujenzi wa kivuko hicho, Mwenyekiti wa kamati ya Ujenzi Brazard Mkwizu, amesema kuwa mradi wa ujenzi wa kivuko uliibuliwa na walengwa hao, kutokana na adha kubwa waliyokuwa wakiipata wananchi wa eneo hilo kwa kukosekana kivuko, na kuwasilishwa halmashauri, hatimaye TASAF.

Mkwizu ameweka wazi kuwa eneo hilo lilikiwa ni eneo hatarishi kwa wananchi wa Moivo, nyakati zote za mwaka, huku wahalifu wakitumia eneo hilo kukaba na kunyang'anya watu mali zao, wengine kubakwa huku wengine wakinusurika kuuwawa.

Hata hivyo wanufaika hao wamethibitisha kuwa licha ya TASAF kutatua changamoto ya kivuko katika eneo lao, lakini walengwa hao wamekuwa wakifanya kazi za muda na kulipwa ujira, pesa ambayo huwasaidia kujikimu kimaisha.

"Tunaishukuru Serikali kwa kutujengea kivuko, kwa kuwa eneo hili lilikiwa ni hatari hasa nyakati za usiku na alfajiri, vibaka waligeuza kichaka cha wanyang'anyi, tunategemea tatizo hili litakwisha, lakini zaidi sisi walengwa tumepata ajira za muda licha ya kuwa pesa si nyingi sana ila sio sawa na kukosa kabisa, tunafanya kazi kwa moyo kwa kuwa kivuko hiki, kitatusaidia wakazi wote wa Moivo". Amesema Tatu Hamisi mnufaika wa mpango wa Kunusuru kaya Masikini.

Naye Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, amewataka wananchi hao kujitoa kwa moyo wakati wote wa ujenzi mpaka kukamilika kwa kivuko hicho, huku akiwasisitiza kukitunza mara baada ya kukamilika.

"Mnapaswa kutambua namna Serikali inawathamini na kutatua kero iliyokuwa inawakabili, rai yangu ni kutunza miundo mbinu ya kivuko hiki kwa kuwa Serikali inatumia fedha nyingi katika kutekeleza miradi, wananchi mnapaswa kuithamini miradi yote" amesisitiza Msumi.

Awali TASAF imetoa kiasi cha shilingi milioni 76 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kivuko, huku shilingi milioni 38 zikitumika katika ujenzi na milioni 38 zikitumika kulipa ujira kwa wanakaya walio kwenye mpango wa kunusuru kaya masikini katika kijiji hicho cha Moivo, kwa kufanya kazi za muda kwa masaa na kwa zamu kila siku.





Watoto wa shule ya Msingi Oligilai, wakitoa ujumbe wa siku ya Mtoto wa Afrika, wakati wa maadhimisho ya siku yao maalum kupitia ngoma,kwenye viwanja vya shule ya Msingi Sekei.

# JAMII YAASWA KUTOFUMBIA MACHO VITENDO VYA UKATILI DHIDI YA WATOTO

Na Elinipa Lupembe

Katika kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, Jamii imetakiwa kutokufumbia macho matukio ya ukatili dhidi ya watoto na kutakiwa kushirikiana na viongozi wa Serikali, kuwafichua watu wahalifu ukatili kwa watoto kwa kutoa taarifa mapema, pindi tu haki ya mtoto inapokiukwa ili kupunguza idadi ya matukio ya ukatili kwa watoto.

Rai hiyo imetolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha Mhe. Ojung'u Salekwa, wakati wa maadhimisho ya siku ya mtoto wa Afrika katika halmashauri hiyo, yaliyofanyika kwenye viwanja vya shule ya Msingi Sekei.

Mwenyekiti Ojung'u ameweka wazi kuwa, tafiti zinaonesha kuwa, matukio mengi ya ukatili kwa watoto, yanafanyika ndani ya familia zetu na ndugu wa karibu, na jamii inashindwa kuwafichua watuhumiwa hao, kutokana na mahusiano ya undugu katika familia, hivyo ni vema jamii kutambua athari wanazozipata watoto kutokana na matukio hayo, na kuamua kuchukua hatua kama ilivyo makusudio ya serikali.

"Ni wajibu wetu kama viongozi kuwakumbusha wazazi na jamii kutekeleza wajibu wao kwa Watoto, kuwalinda, kuwasikiliza, kuwapa mahitaji yao ya msingi, pamoja na kuwapa taarifa sahihi juu ya ukatili na kuwawezesha kutoa taarifa pindi watakapofanyiwa vitendo hivyo" amesisitiza mhe. Salekwa.

Aidha, Diwani wa Viti Maalum kata ya Kiutu Mh. Nina Masanja amesema kuwa Watoto wote wana haki ya kupata lishe bora, elimu, malazi pamoja na kutobaguliwa na kutoa wito kwa wazazi kuzingatia upendo kwa Watoto wao na kuwapa elimu juu ya vitendo vya kikatili dhidi yao.

"Ukatili wa aina yoyote dhidi ya mtoto haukubaliki kabisa katika jamii yetu, tushirikiane kwa pamoja kutoa taarifa katika vituo Maalum au kupitia namba maalum 116,kwa kufanya hivyo vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vitapungua mpaka kuisha kabisa" amebainisha Mheshimiwa Nina.

Hata hivyo Watoto waliojumuika katika kuadhimisha siku yao muhimu ya Mtoto wa Afrika, wameiomba Serikali kufuatilia kwa ukaribu zaidi ili kubaini matukio ya kikatili yanayofanyika katika jamii inayowazunguka na wale wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya kikatili dhidi ya Watoto wachukuliwe hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine.

Naye Afisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Arusha, Getruda Darema, ameweka wazi kuwa, halmashauri ya Arusha kwa kushirkina na wadau, inatekeleza mikakati ya kuimarisha ulinzi na usalama wa mtoto kupitia Klabu za watoto shuleni, kamati za MTAKUWWA kuanzia ngazi ya vijiji, pamoja na kutoa mafunzo kwa makundi mbalimbali katika jamii ikiwemo vijana, wanawake, wazee na viongozi wa dini na mila.

Maadhimisho ya siku ya mtoto wa Afrika 2022 yenye Kaulimbiu ya "Tuimarishe ulinzi kwa mtoto; Tokomeza ukatili dhidi yake: Jiandae kuhesabiwa", lengo likiwa ni kuendelea kupambana kupinga ukatili dhidi ya Watoto kwa kuijengea jamii uelewa wa pamoja juu haki za msingi za mtoto.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha Mhe. Ojung'u Salekwa, akifungua Mkutano wa Baraza la Madiwani

# WAATHIRIKA WA VVU WASHAURIWA KUACHANA NA IMANI POTOFU BADALA YAKE KUENDELEA KUTUMIA ARV

Waathirika wa virusi ya UKIMWI, wameshauriwa kuachana na imani potofu, zinazowasababisha kuacha, kutumia dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI - ARV.

Rai hiyo imetolewa wakati wa mkutano wa Baraza la Madiwani wa robo ya tatu mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Arusha, mkutano uliofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa halmashauri hiyo.

Akizungumza wakati wa kipindi cha maswali ya papo kwa papo, Diwani wa Kata ya Kimnyaki Mhe. Eliakimu Marivey, amehoji juu ya mkakati wa halmashauti kwa watu wanoishi na virusi vya UKIMWI, na kuacha kutumia dawa za kufubaza virusi hivyo, kutokana na imani potofu zinazotokana na mila na desturi.

Akijibu swali hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Selemani Msumi ameweka wazi kuwa, Serikali kupitia watalamu wa sekta zote, inaendelea kutoa elimu kwa jamii, juu ya umuhimu wa vidonge vya kufubaza makali ya Virusi vya UKIMWI, na kuwataka viongozi wa mila na dini kushiriki kutoa elimu sahihi kwa waumini wao kuhusu matumizi ya dawa hizo.

"Mara nyingi watu wamekuwa wakisitisha matumizi ya Dawa za Magonjwa kama Pressure na UKIMWI kwa madai ya kuchoshwa na dawa hizo pamoja na imani potofu, badala yake wanatumia dawa za miti shamba, hali inayopelekea kufupisha Maisha yao, niwaombe viongozi wenzangu tushirikiane kuelemisha jamii katika maeneo yetu". Amesisitiza Msumi.

Hata hivyo baadhi ya wajumbe wameahidi kuendelea kushirikiana na Serikali kutoa elimu kwa jamii na kuifanya agenda ya kudumu kwenye mikutano ya vijiji, lengo likiwa ni kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa za ARVs pamoja na umuhimu wa dawa hizo kwa maisha.



Mh. Eliakimu Marivey
Diwani wa Kata ya Kimnyaki

"Ninawashauri watu wenye maambukizi waendelee kutumia ARV, kuacha kutumia dawa hizo ni kuhatarisha maisha ya mtu binafsi, pia na wale watakaobainika kutoa elimu isiyo sahihi Serikali iwachukulie hatua za kisheria.". Amesema Mhe. Elinipa Laizer, Diwani Viti Maalum CCM.

Mkutano huo wa Baraza la Madiwani umejikita kujadili utekelezaji wa shughuli za halmashauri, ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo kiseta, mapato na matumizi pamoja na shughuli za maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii zilizotekelezwa katika maeneo yote ndani ya Halmashauri katika kipindi cha robo ya tatu ya kuanzia mwezi Januari hadi Machi 2022.





Mwl. James Mchembe, Katibu Tawala Wilaya ya Arumeru

# WALIMU WAAGIZWA KUSIMAMIA KILA MWANAFUNZI KUOTESHA MTI NA KUUTUNZA AWAPO SHULENI

Na Elinipa Lupembe

Halmashauri ya Arusha, imeadhimisha kilele cha siku ya Mazingira Duniani mwaka 2022, kwa kuwataka wakazi wa halmashauri hiyo, kutunza mazingira kwa kupanda miti huku walimu wakisisitizwa kuhakikisha kila mwanafunzi anaotesha mti shuleni kwakwe na kuutunza mpaka atakapohitimu masomo yake shuleni hapo.

Rai hiyo imetolewa na mgeni rasmi, kwa niaba ya mkuu wa wilaya ya Arumeru, Katibu Tawala wa willaya hiyo, Mwalimu James Mchembe, wakati akizungumza na wananchi kwenye kilele cha maadhimisho ya wiki ya Mazingira Duniani, yaliyofanyika kwenye viwanja vya shule ya msingi Nduruma, kata ya Nduruma.

Katibu Tawala huyo ameweka wazi kuwa, umuhimu wa kutunza mazingira ni pamoja na kupanda miti, na kuwataka walimu kuwasimamia wanafunzi katika shule zao, kwa kuhakisha kila mwanafunzi anapanda mti mmoja na kuutunza mpaka atakapohitimu masomo yake katika shule husika.

"Kama kila mwanafunzi atapanda mti, tutakuwa na miti mingi katika maeneo yetu, lakini zaidi miti ya matunda itawapatia watoto lishe itakayotokana na mazao ya miti hiyo ya matunda watakayoipanda, niwasihi walimu kila mwanafunzi awe na mti wake na ndio alama atakayoiacha shuleni." Amesistiza Mwl. Mchembe.

Hata hivyo Katibu Tawala huyo, alimnukuu mwandishi mmoja wa kitabu, aliyesema moja kati ya mambo matatu muhimu yanayoweza kumfanya binadamu akaacha kumbukumbu katika historia ya maisha yake duniani ni kupanda mti, na kusisitiza kuwa kila mtu anawajibu wa kuacha kumbukumbu kwenye mazingira yake kwa kupanda mti.

Naye Mwenyekiti wa halmashauri ya Arusha Mhe. Ojung'u Salekwa amesema kila mwananchi analo jukumu la kutunza mazingira, kutokana na ukweli kwamba, uharibifu wa mazingira umesababisha madhara makubwa duniani, ikiwemo uhaba wa mvua na ongezeko la joto duniani madhara ambayo tayari yanaonekana dhahiri katika maisha yetu.

Aidha amewata wataalamu wa Mazingira kuendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii, hususani wanafunzi, ili wafahamu umuhimu wa kutunza mazingira, zaidi wawe na nasaba na



na mazingira yao, jambo ambalo litaleta matokeo chanya.

Awali Mkuu wa Idara ya Mazingira halmashauri ya Arusha, Zuraika Mkundya, licha ya juhudi kubwa inayofanywa na idara hiyo kwa kushirikiana na wadau, bado kuna changamoto ya ushiriki mdogo wa baadhi ya viongozi unaosababisha migogoro ya kimazingira, uchafuzi na uharibifu wa hifadhi za mazingira.

Katika kuadhimisha kilele cha wiki ya mazingira duniani, yenye kauli mbiu, Tanzania ni Moja, Tunza Mazingira, halmashauri imepanda jumla ya miti mia tisa, katika shule za kata ya Nduruma.





Jaykany Shan, mfadhili

# WAFADHILI WAAHIDI KUSHIRIKIANA NA SERIKALI YA TANZANIA KATIKA SEKTA YA ELIMU

Wafadhili wa Jaykat Shah Foundation na Made with Hope wa nchini Uingereza, kwa kushirikiana na shirika la Ndoto in Action la nchini, wameahidi kuendelea kushirikiana na serikali ya Tanzania kwa kutatua changamoto za jamii hususani katika sekta ya elimu.

Wafadhili hao Jaykany Shah na Alexander Margolin kwa pamoja, wamefikia uamuzi huo, mara baada ya kukagua utekelezaji wa miradi wanayoifadhili inayotekelezwa na shirika la Ndoto in Action, ikiwemo ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi Mshikamano na Marurani, kata ya Nduruma halmashauri ya Arusha.

Aidha katika ziara hiyo, wafadhili hao wameshiriki hafla ya makabidhiano ya vyumba 11 vya madarasa vilivyofanyiwa ukarabati mkubwa, madawadi 65, miundombinu ya kuvuna maji, miradi iliyogharimu shilingi milioni 75, na kutekelezwa na shirika la Ndoto in Action katika shule ya msingi Marurani na kuahidi kuendelea kufadhili miradi katika shule nyingine za msingi kutokana na uhitaji mkubwa waliuona.

"Lengo letu ni kusaidia jamii ya watanzania, hasa watoto kusoma katika mazingira rafiki, tumeridhishwa na miradi iliyofanyika na kuona inasaidia watoto tuliowakusudia, tunaahidi kuendela kutoa 'support' zaidi, ili watoto wakitanzania wapate elimu katika mazingira bora." Amesisitiza Jaykhan

Akizungumza wakati wa kukabidhi mradi huo, mkurugenzi wa shirika la Ndoto in Action, Hussein Hassan, amesema, shirika linashukuru kwa ushirikiano wanaoupata kutoka kwa serikali na shirika linaunga mkono juhudi na kasi ya maendeleo inayofanywa na serikali ya awamu ya sita, kwa kuboresha sekta ya elimu na kuweka mazingira rafiki shuleni.

"Shirika linatambua changamoto ya miundombinu inayozibili shule nyingi nchini ikiwemo upungufu wa vyumba vya madarasa, uchakavu wa majengo, upungufu wa madawati, miundombinu ya vyoo pamoja na maji, vifaa vya kisasa vya kufundishia licha ya juhudi kubwa inayofanywa na serikali, kuboresha miundombinu ya shule, sisi tuko bega kwa bega na serikali." Ameweka wazi Hussein

Naye Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, kadhalika amewashukuru wafadhili hao, kwa kukarabati miundombinu ya shule ya msingi Marurani, na kuwataka walimu na wanafunzi kuendelea kuitunza miundombinu hiyo ili iweze kuwasidia kama yalivyokuwa malengo ya wafadhili hao na serikali pia.

"Serikali inatambua na kuthamini michango ya wadau wa maendeleo kwa kuwa wanafanya kwa niaba ya serikali, walimu, wanafunzi na wazazi tunalo deni la kurejesha fadhila kwa wafadhili hawa, inatubidi kuhimiza watoto wetu kusoma kwa bidii, pamoja na kutunza miundombinu hii, walimu hakikisheni wanafunzi wanatumia miundombinu yote kwa utaratibu unaofaa." Amesisitiza Mkurugenzi Msumi.

Aidha wanafunzi wa shule ya msingi Marurani, licha ya kuwashukuru wafadhili waliotekeleza mradi huo, wamethibitisha mradi huo utawaongezea ari ya kusoma kwa bidii, kwenye mazingira rafiki na kupandisha kiwango cha taaluma shuleni hapo, huku wakiahidi kufaulu katika masomo yao.

Hata hivyo mwalimu mkuu wa shule ya Msingi Marurani, amethibitisha kupanda kwa kiwango cha taaluma shuleni hapo, na kuongeza kuwa kwa miaka mitatu mfululizo sasa shule inafanya vizuri kwa kushika nafasi za juu kitaaluma kuanzia ngazi ya kata, wilaya, mkoa na hata ngazi ya Taifa.

Ikumbukwe kuwa awali, shirika la Ndoto in Action, lilifanya ukarabati wa vyumba 4 vya madarasa, ujenzi wa choo cha wasichana chenye sehemu ya kujisitiri wasichana wakati wa hedhi, na kuongeza maadarasa 11 na kukamilisha ukarabati wa jumla ya madarasa 15, katika shule ya msingi Marurani yenye jumla ya wanafunzi 424.



Walimu Shule za Msingi wakiwa kwenye Semina ya Mafunzo ya Walimu Kazini

# WALIMU WAHIMIZWA KUJISOMEA KUPITIA PROGRAMU YA MEWAKA

Na Elinipa Lupembe

Walimu halmashauri ya Arusha, wametakiwa kutumia fursa inayotolewa na Serikali ya kupitia programu ya Mafunzo Endelevu kwa Walimu Kazini (MEWAKA), mafunzo yenye lengo la kuboresha utaalamu kitaaluma kwa walimu, ili kuwa mahiri katika mbinu za ufundishaji zinazoendana na wakati.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mtendaji, halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, wakati akifungua Semina ya Mafunzo ya Walimu Kazini, iliyojumuisha walimu wakuu wa shule za msingi pamoja na Maafisa Elimu wa kata zote za halmashauri hiyo, semina iliyofanyika kwenye Ukumbi wa shule ya Msingi Green Acress.

Mkurugenzi Msumi, amewataka walimu hao, kutumia fursa hiyo, inayotolewa na Serikali kuhakikisha wanapanga muda wa kujifunza zaidi kupitia miongozo na utaalam uliotolewa kwenye moduli za MEWAKA, mafunzo ambayo yatawawezesha kupata maarifa mapya na mbinu shirikishi za ufundishaji, pamoja na kufanya tathmini kwa wanafunzi.

"Serikali inatambua na inathamini kazi kubwa inayofanywa na walimu, na kuona umuhimu wa kuandaa mkakati wa MEWAKA, utakowewezesha kapata mafunzo kazini, hivyo nitoe wito kwenu viongozi wa shule, kuratibu na kusimamia mpango huo katika maeneo yenu ya kazi, ili kufikia malengo ya serikali ya kuinua kiwango cha taaluma shuleni" amesisitiza Mkurugenzi Msumi.

Naye Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi halmashauri ya Arusha, Salvatory Alute, amefafanua kuwa, lengo la semina hiyo kwa viongozi hao wa elimu ngazi ya kata na shule ni kuwajengea uwezo wa kuratibu na kusimamia programu ya MEWAKA katika maeneo yao ya kazi, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kuwa wathibiti ubora wa ndani ya shule, kufuatilia utekelezaji wa MEWAKA na kufanya tathmini, kuwawezesha wadau wa elimu katika kupanga gharama za uendeshaji wa mafunzo na upatikanaji wa rasilimali pamoja na usimamizi wa rasilimali hizo.

Hata hivyo Afisa Elimu huyo, amebainisha kuwa mfumo wa MEWAKA umeondoa changamoto nyingi zilizokuwepo za mifumo iliyotumika hapo awali ya mafunzo kwa walimu, hivyo programu ya MEWAKA ni mfumo rasmi ambao umeandaliwa na Serikali kutekeleza mtaala wa elimu msingi, unaozingatia umahiri wa mbinu za kufundishia na kujifunzia, kufanya tathmini kwa wanafunzi, pamoja na kuendeleza mafunzo hayo kwa kuhawilisha taaluma kwa walimu wote.

"MEWAKA imeandaliwa na Taasisi ya Elimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, kwa kuzingatia mitaala ya elimu inaozingatia umahiri, ndani yake kuna moduli mbalimbali zitakazowawezesha walimu kujinoa kitaaluma na kuwa mahiri katika ufundishaji pamoja na kujifunza namna ya kuendeleza mafunzo hayo kwa walimu wote ili kuwa na umahiri unaoendana na wakati." Amefafanua Afisa Elimu Alute.

Aidha walimu hao wameweka wazi kuwa, MEWAKA imekuja wakati muafaka, kutokana na kasi ya maendeleo ya kisayansi, yanayotokana na mabadiliko ya teknolojia, mabadiliko yanayomlazimu mwalimu kujisomea sana ili kupata maarifa mapya, huku wakithibitisha kuwa, program ya MEWAKA, inawapa walimu fursa endelevu ua kujinoa kitaaluma kwa kusoma na kubadilishana uzoefu wa kazi.

Mwalimu Mkuu, shule ya Msingi Ngaramtoni, mwalimu Makanjo Twaty, amesema kuwa program ya MEWAKA ni muhimu kwa walimu, na watahakikishia kutumiammuda wa ziada kujifunza miongo yote iliyoainishwa bila kuathiri ratiba za masomo kwa wanafunzi, huku akisistiza kuwa MEWAKA itawafanya walimu kufundisha kwa kuendana na wakati, hasa kwa walimu waliosoma miaka mingi iliyopita.

"Kwa mwalimu kama mimi, niliyeanza kazi miaka ya 80, nisiposoma ninapitwa na wakati kabisa, lakini kupitia MEWAKA kila mwlaimu atalazimika kujisomea na kupata maarifa mapya, yatakayotuwezesha kwenda na wakati, munaotokana na mabadiliko ya teknolojia" ameweka wazi Mwalimu Twaty.

Awali matarajio ya programu ya Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini, ni kuwawezesha walimu kufanyakazi kwa weledi, kusaidiana, kushirikiana, kutoa maoni kiuzoefu na kistadi katika ufunzaji na ufundishaji, kuinua matokeo ya ujifunzaji kwa wanafunzi pamoja ma kuwezesha umiliki kwa kile ambacho walimu wanajifunza kwa kuwa wanapata ya kupanga na kuamua nini cha kujifunza na kwa wakati gani.



Ujenzi wa Mabweni ya Wavulana Shule ya Sekondari Oldonyowas

# BAADA YA BWENI LA WASICHANA, TASAF YAWAKUMBUKA WAVULANA SEKONDARI OLDONYOWAS.

Na Elinipa Lupembe

Katika kutekeleza mkakati wa kuboresha miundombinu ya shule, serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), imewakumbuka wavulana wa shule ya sekondari Oldonyowas, kwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa mabweni mawili ya wavulana shule ya sekondari Oldonywas, halmashauri ya Arusha, baada ya kujenga mabweni mawili ya wasichana shuleni hapo.

Akizungumza wakati wa kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo, mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, ameweka wazi kuwa, kwa mara nyingine tena, serikali kupitia mfuko wa TASAF imetoa fedha, kiasi cha shilingi milioni 320, kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili ya kulala wanafunzi wavulana 160, ikiwa ni baada ya awamu ya kwanza kujenga mabweni mengine mawili ya wasichana kwa shule hiyo.

Mkurugenzi Msumi amethibitisha umuhimu wa shule hiyo kuwa na mabweni kwa wanafunzi wa jinsi zote, ni kutokana na asili ya mazingira ya eneo hilo, watoto wengi wanaishi mbali na shule na kusababisha kutembea umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni, jambo ambalo linawaathiri kiafya, kisaikolojia na hata kitaaluma.

"Ninampongeza Rais wetu, Mama Samia kwa kusikia kilio cha watoto wake, watoto wa Oldonyowas, na kujenga mabweni ya wavulana pia, tunaamini uwepo wa mabweni utaongeza ari ya wanafunzi kupenda shule, kutapunguza watoto kuacha shule, kwa kuwa na mazingira tulivu ya kujisomea, jambo ambalo litapandisha taaluma shuleni na kuongeza kiwango ya ufaulu kwa wanafunzi." Amefafanua Mkurugenzi Msumi

Naye Michael Ismail mwanafunzi wa kidato cha nne, licha ya kuishukuru serikali ya awamu ya sita, amekiri kufurahishwa na kitendo cha kujengwa mabweni ya wavulana shuleni hapo, ambapo awali kulikuwa na mabweni ya wasichana pekee, na kuongeza kuwa wanafunzi wengi hukosa muda wa kujisomea wawapo nyumbani, kutokana na uchovu wa kutembea umbali mrefu, huku wazazi wakiwapangia majukumu ya kazi za nyumbani mara watokapo shuleni.

"Watoto wengi wanaishi mbali na shule lakini wakifika nyumba watapewa kazi za kuchunga ama kuhudumia mifugo, jambo linalotukosesha muda wa ziada wa kujisomea tuwapo nyumbani, lakini uwepo wa mabweni utatusaidia kutumia muda mwingi kujisomea kwa pamoja na kuturahisishia kufanya kazi za shule kwa kujadiliana katika makundi 'group discussion'." Amefafanua mwanafunzi Michael

Mradi huo wa ujenzi wa mabweni mawili ya wavulana shule ya sekondari Oldonyowas, unafanya kuwa na idadi ya miradi tisa tofauti iliyotekelezwa na TASAF katika shule hiyo, ikiwemo vyumba vya madarasa, mabweni mawili ya wasichana, jengo la utawala, matundu ya vyoo na nyumba za walimu.







Pichani kushoto: Mkurugenzi wa Opec Fund Duniani Dkt. Alkhalifa Abdulhamid Saleh akikagua nyumba ya Walimu

# MKURUGENZI WA OPEC FUND ARIDHISHWA NA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA TASAF NCHINI

Na Elinipa Lupembe

Mkurugenzi wa Umoja wa Nchi zinazozalisha Mafuta kwa wingi Duniani (Opec Fund), Dkt. Alkhalifa Abdulhamid Saleh, ameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na kuthibitisha kuwa umoja huo utaendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania kuhakikisha, miradi yote iliyofadhiliwa na OPEC FUND, inakamilika kwa wakati na kuleta matokeo chanya kwa jamii.

Amesema hayo wakati akikagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na TASAF awamu ya III na ya IV, katika shule ya sekondari Oldonyowas, halmashauri ya Arusha, wilaya ni Arumeru, mkoa wa Arusha.

"Tunaishukuru serikali ya Tanzania kwa kushirikiana nasi, kutekeleza miradi ya maendeleo ya kuondoa umasikini katika sekta ya elimu na afya, nimefurahi kuona watoto wanasoma katika mazingira bora, madarasa mazuri na mabweni mazuri, shule ina jengo zuri la utawala pamoja na nyumba nzuri za walimu" amesistiza Dkt. Alkhalifa

Aidha, Dkt. Alkhalifa ameongeza kuwa, malengo ya serikali kuanzia mwaka 2020 -2025, ni kuhakikisha inapeleka maendeleo kwa kasi kwa wananchi lengo likiwa ni kukabiliana na wimbi la umasiki uliokithiri, kuwezesha kaya kupata huduma za afya na elimu pamoja na kukuza pato la familia kwa maendeleo ya jamii nzima.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF Tanzania, Ladislaus Mwamanga, amesema kuwa, ugeni kutoka OPEC FUND, umekuja kufanya mapitio ya kawaida pamoja na kufanya tathimini ya miradi iliyotekekelezwa na fedha kutoa OPEC FUND.

"Umoja huo unashirikiana na serikali ya Tanzania kuchangia miradi ya maendeleo kwa wananchi kwa ajili ya kupunguza wimbi la umasikini katika jamii, wamekuja kuona miradi hiyo, na wameridhishwa na utekelezaji wa miradi ikiwemo ujenzi wa miundombinu ambayo inawasaidia wanafunzi, kwa kuwa wanapata huduma zote za msingi shuleni".Amesema Mkurugenzi Mwamanga.

Mkurugenzi Mwamanga, amefafanua kuwa, viongozi wa OPEC walipokutana na Mheshimwa Rais Samia Suluhu Hassan, walitoa mkopo wa dola za Kimarekani milioni 50 sawa na shilingi bilioni 120, kwa ajili ya kuendeleza mradi wa kupunguza umasikini awamu ya nne, mradi ambao unatekelezwa katika mikoa mitano ya Tanzania Bara ambayo ni Arusha Njombe, Simiyu, Mwanza na Geita.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Oldonyowas, Mhe. Godfray Ayo, ameushukuru Uongozi wa OPEC kupitia TASAF, kwa kutoa fedha, ambazo zimewezesha ujenzi wa miundombinu ya shule ya sekondari Oldonyowas, pamoja na fedha za kupunguza umaskini kwa wananchi wa eneo hilo, huku akiweka wazi kuwa kijiji chake pekee kimepata jumla ya shilingi milioni 747.7.

"Wananchi wamenufaika na miradi inayotekelezwa na TASAF, kwa kuwa hali ya umaskini uliokithiri imeanza kupungua katika kijiji chetu, watoto wetu wanaendelea na masomo ya sekondari, wananchi sasa wanafanya mifugo biashara, huku wengine wakinufaika na mpango wa kuhawilisha fedha."Amesisitiza Mwenyekiti huyo.

Awali Kijiji cha Oldonyowas pekee kimetekeleza jumla ya miradi sita yenye thamani ya shilingi milioni 747.7, milioni 34 zimetekeleza mradi wa ufugaji kuku chotara, milioni 97.8 ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo, milioni 76.7 nyumba za walimu, milioni 104 jengo la Utawala, milioni 175.1 mabweni mawili ya wasichana, na ujenzi wa mabweni mawili ya wavulana utakaoghatimu shilingi milioni 338.7 Kwa TASAF III awamu ya pili.






Wanufaika wa TASAF wakiwa kwenye bishara zao ndogondogo

# VIKUNDI VYA WALENGWA WA TASAF VYAINUA UCHUMI WA KAYA

Na Elinipa Lupembe

Wanufaika wa mpango wa Kunusuru Kaya Masikini, mradi unaotekelezwa Serikali kupitia Mfuko wa Maendelo ya Jamii (TASAF III) awamu ya pili, wameanza kunufaika kiuchumi kupitia vikundi vya kuweka na kuwekeza, vikundi vilivyoviunda na walengwa hao, halmashauri ya Arusha.

Walengwa hao wa kijiji cha Oltulelei kata ya Ilboru, wameweza kuinua vipato vya familia zao kwa kujipatia mitaji ya kuanzisha miradi midogo midogo, kupitia programu ya vikundi vya TASAF vya kuweka, kuwekeza na kukopa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye maeneo wanayofanyia biashara, wana kaya hao wamethibitisha kuwa, licha ya kupokea fedha za ruzuku ya mwezi kutoka TASAF, lakini pia walijengewa uwezo wa kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa kupitia fedha za ruzuku wanazopokea.

Janeth John mlengwa na mwenyekiti wa kikundi cha UPENDO -TASAF anayemiliki genge la kuuza mbogamboaga kwa sasa, amesema kuwa watalamu waliwajengea uwezo wa kuanzisha vikundi vya kuwekeza, kutokana na pesa ya ruzuku wanayoipa kutoka TASAF, na baada ya kuanzisha kikundi kimewawezesha kupata mitaji na kuongeza kuwa kila mwanakukundi ameshaanzisha biashara yake sasa.

Amefafanua kuwa kikundi chao kina wana wanachama 10, mwanzo walikuwa na hofu lakini wameweza kupata mitaji ya kuanzisha biashara, ambazo zimepunguza ugumu wa maisha, kuwekeza, kukopa na kurejesha kwa wakati, na kukiri kuwa, walipoanza kikundi wengi wao hawakuwa na biashara, ila kwa sasa wanachama wote 10 wanajishughulisha na biashara ndogondogo.

“Hapo mwanzo hatukuamini kama jambo hili litawezekana, kutoka na kiasi kidogo cha pesa tunachopokea, lakini tumeweza kugonga hisa kila wiki, tuna mfuko wa jamii ambao unasaidia kutatua changamoto za kijamii ikiwemo msiba na ugonjwa, lakini zaidi tumeweza kukopeshana na kupata mitaji, inayotuwezesha kuendelea kuweka akiba, kukopa na kupata marejesho, huku faida ya biashara ikituwezesha kuhudumia familia zetu.” Amesisitiza Janeth.


Rabisante Mwanga, mwanakikundi cha UPENDO na mama wa watoto watatu, amebainisha kuwa, kupitia kikundi chao cha UPENDO TASAF, ameweza kupata mtaji wa shilingi 150,000 wa kuuza mitumba, mradi ambao unampatia kipato cha kumudu maisha na familia yake huku akiwa na matarajio ya kukuza mtaji na kuanza kununua mitumba kwa jumla maarufu kama 'beli'.

Dina Yoram, mlengwa anayemiliki genge na sehemu ya kuchoma samaki na mihogo, ameweka wazi kunufaika na kikundi na ameweza kuongeza kipato cha familia yake, na kumfanya kumudu mahitaji ya muhimu kwa familia na kuwataka wanawake wasibweteke badala yake, kutumia fursa hizo za kujiunga kwenye vikundi vya kuweka na kukuopa ili kupata mitaji ya kuanzisha biashara.

Hata hivyo Dina Emson, amewaka wazi kuwa kabla ya kuanza kupokea pesa za TASAF alikuwa na ujuzi wa kusuka, akisuka wateja wake kwenye eneo lisilo rasmi, baada ya kujiunga na kikundi cha TASAF amefanikiwa kufungua saloon, eneo ambalo limemuwezesha kupata wateja zaidi.

"Nilikuwa na ujuzi wa kusuka nawafuata wateja nyumbani, jambo ambalo lilinigharimu nauli ya kwenda na kurudi, kwa sasa wateja wangu wananifuata hapa saloon kwangu, kadri siku zinavyokwenda natarajia kuweka vifaa vya kisasa zaidi ili kupata wateja zaidi na faida." Amesistiza Upendo.

Mpango wa Kunusuru kaya masikini, wenye lengo la kukuza pato la familia, umekuwa na programu ya vikundi vya kuweka na kuwekeza kwa walengwa walio kwenye mpango ili kukuza uchumi wa kaya, program ambayo imeanza kuzaa matunda kwa baadhi ya Kaya za walengwa.





DC Arumeru Mhandisi Richard Ruyango akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa wilaya ya Arusha Mhe. Said Mtanda

# MAPOKEZI YA MWENGE WA UHURU HALMASHAURI YA ARUSHA 2022

Na Elinipa Lupembe

Mkuu wa wilaya ya Arumeru Mhandisi Richard Ruyango amepokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa wilaya ya Arusha Mhe. Said Mtanda tarehe 23.06.2022, kwenye viwanja vya shule ya sekondari Oldadai, halmashauri ya Arusha.

Mhandisi Ruyango, amebainisha kuwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2022, ndugu Sahil Nyanzabara Geraruma amekimbiza Mwenge wa Uhuru Kilomita 90.4, na kupitia jumla ya Miradi 9 yenye thamani ya shilingi Bilioni 4.2 kwenye sekta ya elimu, afya, maji, miundombinu ya barabara na uwekezaji.



Aidha Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, ametembelea shule ya sekondari Oldadai na kikagua mradi wa ukamilishaji ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, kuzindua ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, pamoja na kuzinduzi Muungano wa Klabu ya Wapinga rusha na Skauti (SKUTA).

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru ametembe miradi ujenzi wa mradi wa maji wa vijiji 5, kijiji cha Losikito, kata ya Mwandeti, amezindua Mradi wa Uwekezaji kiwanda cha Maziwa SIVAT pamoja na kitembelea Nyumba maalum ya Warahibu wa Madawa ya kulevya kata ya Olturumet na kituo cha kutoa virutubisho kwa watoto wenye utapiamlo kata ya Mateves.

Mwenge wa Uhuru umetembelea mradi Kikundi cha Vijana (WINNER STUNNA) kilichopewa mkopo wa asilimi 4 ya vijana kiasi cha shilingi milioni 10, fedha za Mapato ya ndani ya Halmashauri, umezindua mradi wa ujenzi wa barabara ya Martenity Africa wenye thamani ya shilingi milioni 897 fedha kutoka Serikali Kuu na kuweka jiwe la Msingi kwenye kituo cha Afya Oloirieni.

Mwenge wa Uhuru ulikesha kwenye viwanja vya Makao Makuu ya Halmashauri ya Arusha, eneo la Sekei kata ya Kiutu, na kisha kukabidhiwa kwenye halmashauri ya Meru wilaya ya Arumeru.






Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa ndugu Sahili Nyanzabara Geraruma alipotembelea Kikundi cha Vijana Winner Stunna.

# KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA AMEWATAKA VIJANA KUTUMIA FURSA YA MIKOPO ISIYO NA RIBA INAYOTOLEWA NA HALMASHAURI

Na Elinipa Lupembe

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Ndg. Salihi Geraruma, amewataka vijana kuwacha tabia ya kulalamika maisha magumu, badala yake kujishughulisha kwa kufanya kazi kwa bidii, sambamba na kutumia fursa za uwezeshwaji kupitia asilimia 4 ya mikopo isiyo na riba, inayotolewa na halmashauri zote nchini.

Kiongozi huyo, amesema hayo wakati Mwenge wa Uhuru ulipotembelea Kikundi cha Vijana cha Winner Stunna, wanaojishughulisha na ufundi selemala na kupewa mkopo wa shilingi milioni 10 kupitia mapato ya ndani ya halmashauri ya Arusha.

Licha ya kuwapongeza vijana amewasisitiza kufanya kazi kwa bidii, ili waweze kurejesha mkopo huo, ikiwa ni pamoja na kutengenza bidhaa zenye ubora ili kukabiliana na ushindani wa soko, ikiwa ni pamoja na kutafuta kazi zinazotolewa na Serikali.

Hata hivyo amewaagiza watalamu wa halmashuri hiyo, kuwa karibu na vijana hao kwa kuwawezesha kupata kazi zinazotolewa na halmashauri ikiwemo kuwa na mashine ya risiti ya mlipa kodi kutoka TRA 'EFD'.

"Wasaidieni vijana hawa kupata mashine ya EFD ili muweze kuwapa kazi zinaotolewa na halmashauri, jambo ambalo litawawezesha biashara zao kukua, kuwakopesa tu haitoshi, lazima kuwapa mbinu zaidi za kufanya biashara". Amesisitiza Kiongozi huyo

Mwenge wa Uhuru 2022, wenye kauli mbiu ya Sensa ni Msingi wa Mipango ya Maendeleo, Shiriki kuhesabiwa Tuyafikie Maendeleo.







Mwenyekiti Halmashauri ya Arusha, Mhe. Ojung'u Salekwa (katikati) alipotembelea Zahanati ya Imbibya

# MWENYEKITI ARUSHA DC, AITAKA JAMII KUWAHUDUMIA WAJAWAZITO

Na Elinipa Lupembe

Jamii imetakiwa kuwahudumia kina mama wajawazito kwa, kwa kuhakikisha wanahudhuria kliniki na kupatiwa lishe bora kwa siku 1000 za ujauzito, huku ikisisitizwa wajawazito kujifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na sio nyumbani.

Rai hiyo imetolewa na Mwenyekiti halmasahuri ya Arusha, na Diwani wa Kata ya Laroi, Mhe. Ojung'u Salekwa, alipotembelea zahanati ya Imbibya kata ya Mwandeti, wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hali ya upatikanaji wa huduma za afya katika halmasahuri yake.

Mwenyekiti Ojung'u licha ya kuridhishwa na upatikanaji wa huduma za afya katika vituo vya afya vya Serikali katika halmashauri hiyo, pia amebaini changamoto za kinamama wajawazito, kutokuhudhuria kliniki kwa wakati, kujifungulia nyumbani na kutokuzingatia lishe bora kwa siku 1000 za ujauzito.

"Tunapaswa kutambua suala la ujauzito ni la familia na jamii nzima, hivyo ni vyema wote kuzingatia kumlea mjazito kwa kuhakikisha anahudhurua Kliniki mara anapohisi ana ujauzito, kumpa lishe bora kwa siku 1000 za ujauzito pamoja na kujifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na si nyumbani" amesisitiza Mwenyekiti Ojong'u

Naye Namyaki Lukumai, amesema kuwa kwa sasa jamii yao imeanza kuelimika juu ya umuhimu wa Wajawazito kuhudhuria Kliniki pamoja na kujifungulia kwenye vituo vya afya tofauti na hapo awali wengi hawakutaka na kuongeza kuwa sio kwamba watu walikuwa hawataki bali hawakuwa na elimu sahihi.

"Serikali iendelee kutoa elimu zaidi na kuhamasisha jamii faida za kuhuduria kliniki pamoja na madhara ya kutokuhuduria kliniki, madhara ambayo wengi wameanza kuyashuhudia ikiwemo vifo vya kinamama wajawazito na watoto wakati wa kujifungua". Amesisitiza Namnyaki

Hata hivyo Mratibu wa Afya ya Uzazi, Muuguzi Bujiku Butolwa amewasisitiza wajawazito kuhudhuria klini na wenza wao, ili wote kwa pamoja wafahamu maendeleo ya afya ya mama na mtoto aliyeko tumboni, pamoja na kupata elimu na ushauri wa utunzaji wa mimba.

Pia mtatibu huyo, amefafanua umuhimu wa mama mjamzito kuhudhuria kliniki kwa wakati ni pamoja na kupata dawa muhimu za kuongeza damu, kuzuia minyoo na malaria, kupima vipimo muhimu, kama uuna tatizo litatuliwe mapema, vipimo hivyo Ni wingi na group la damu, kupata elimu ya Lishe wakati wote wa ujauzito.

Halmashauri ya Arusha inaendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma za Afya ya Mama na Mtoto kwa kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya ikiwemo Zahanati, vituo vya Afya na Hospitali,





DC Arumeru Mhandisi Richard Ruyango (kulia) akimkabidhi mmoja wa Maafisa Kilimo Funguo wa Pikipiki

# SERIKALI YAKABIDHI PIKIPIKI 48 KWA MAAFISA KILIMO ARUSHA DC

Na Elinipa Lupembe

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imetoa pikipiki 48 kwa Maafisa Kilimo, halmashauri ya Arusha, ikiwa ni vitendea kazi kwa Maafisa hao, lengo likiwa ni kuboresha sekta ya Kilimo nchini.

Akizungumza wakati akikabidhi pikipiki hizo, Mkuu wa wilaya ya Arumeru, Mhandisi Richard Ruyango, amewaagiza Maafisa Kilimo kuhakikisha wanatumia pikipiki hizo, kutekeleza majukumu yao kama yalivyo makusudio ya serikali na si vinginevyo.

"Serikali inathamini kazi kubwa mnayoifanya na kuwapa vyombo hivi vya usafiri ili kuwarahisihia utekelazaji wa majukumu yenu kwa wakulima, hatutegemei kuwakuta ofisini, ni jukumu lenu sasa kuwafuata na kuwafikia wakulima kwa haraka na kwa wakati, tunategemea matokeo chanya kwenye sekta ya kilimo katika wailya yetu." Amesisitiza Mhandisi Ruyango.

Naye Mwenyekiti wa halmashauri ya Arusha, Mheshimiwa Ojun'gu Salekwa, amekiri kufarijiwa na serikali ya awamu ya sita, kuwapatia maafisa Kilimo vyombo hivyo vya usafiri, kutokana na mazingira magumu wanayofanyia kazi na kusisitiza kutegemea matokeo chanya kwenye sekta ya kilimo kati halmashauri hiyo.

Hata hivyo mkurugenzi Mtendaji halmasahuri ya Arusha, Seleman Msumi, amewahimiza maafisa hao, kutambua kuwa wamepewa vyombo hivyo vya usafiri kama dhamana, ni muhimu kuvitunza na kuvitumia kwa kazi ya kuwahudumia wakulima katika maeneo yao.

Awali Maafisa ugani hao, wamemshukuru mheshimiwa rais mama Samia Suluhu na kuipongeza serikali yake ya awamu ya sita kwa kuwapatia pikipiki, ikiwa ni kitendea kazi muhimu kwao, kitakachowarahisishia utekelezaji wa majukumu yao hususani kuwafikia wakulima kwa urahisi zaidi.

Afisa Kilimo kata ya Bwawani, Charles Lyakurwa licha ya kumshukuru mama Samia, amebainisha kuwa pikipiki hiyo ni kitendea kazi muhimu sana kwake, kwa kuzingatia kata yake ya Bwawani ina wakulima wengi wenye mashamba makubwa ambao wanahitaji huduma kutoka kwake kama mtaalamu, bila usafiri wa uhakika ilikiwa ni changamoto kuwafikia kwa wingi wao.

Judith Malya Afisa Kilimo kata ya Ilkiding'a amesema kuwa, awali iliwalazimu kutembea hadi umbali wa Kilomita 20 kuwafuata wakulima, uwepo wa pikipiki utarahisisha na kuwafikia wakulima kwa wakati.

Awali Kiamu Mkuu wa Idara ya Kilimo, halmashauri ya Arusha, Bahati Mtweve, amefafanua kuwa jumla ya pikipiki 48 zimekabidhiwa na serikali kupitia wizara ya Kilimo na kukabidhiwa maafisa Ugani wote 48 kwa majina yao ndani ya halmasahuri, lengo likiwa kuboresha sekta ya kilimo nchini.





# MRADI WA BOOST WATUA ARUSHA DC

Na Elinipa Lupembe

Baada ya uzinduzi wa Mradi wa kuboresha upatikanaji wa fursa sawa katika utunzaji bora wa elimu ya awali na msingi Tanzania bara (BOOST) Arusha, timu ya wasimamizi wa mradi huo kitaifa kutoka Wizara ya Elimu, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Bank ya Dunia, hatimaye wamepiga hodi ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, kwa lengo la kujitambulisha na kuanza rasmi utekelezaji wa mradi huo katika halamshauri hiyo.

Katika mazungumzo hayo, timu hiyo ya watalamu, imefafanua kuwa mradi huo wa BOOST unalenga kuimarisha sekta ya elimu ya msingi nchini katika nyanja mbalimbali, kuanzia ngazi ya elimu ya awali, hususani katika maswala ya miundombinu, mpango ambao unatarajiwa kusaidia kuongezeka kwa uwiano wa uandikishwaji wa wanafunzi wa elimu ya awali, pamoja na kuongeza kiwango cha wanafunzi kubaki shuleni

Hata hivyo, Kaim Mkurugenzi halmashauri ya Arusha, mwanasheria Msomi, Monica Mwailolo, baada ya kukamilika kwa mazungumzo na timu hiyo, ameahidi kuwa, halmashauri yake itatekeleza mradi huo kwa weledi na kwa wakati na kuleta matokeo chanya, ili kufikia malengo ya serikali ya awamu ya sita.

Awali, timu hiyo ya watalamu, imefanikiwa kutembea, shule ya msingi Mringa, shule ambayo utekelezaji wa mradi huo umeanza rasmi, katika kipengele cha mafunzo ya walimu.Ikumbukwe kuwa mradi huo wa BOOST, utakoagharimu takriban shilingi Trilioni 1.15, unategemea kutekelezwa nchini kwa kipindi cha miaka mitano na umezinduliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof Adolf Mkenda.




Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mh. John Mongela akizungumza na wafanyakazi wa Mkoa wa Arusha katika madhimisho ya sherehe za Mei Mosi 2022

# RC MONGELA AONGOZA WAFANYAKAZI MKOA WA ARUSHA SHEREHE ZA MEI MOSI 2022

Na Elinipa Lupembe

Mkuu wa mkoa wa Arusha, Mheshimiwa John Mongela amewaongoza wafanyakazi wote wa mkoa wa Arusha, kwenye maadhimisho ya Sikukuu ya Wafanyakazi Mei Mosi, 2022, maadhimisho yaliyofanyika kwenye viwanja vya General Tyre eneo la Njiro, Jijini Arusha.

Mkuu huyo wa mkoa amewapongeza wafanyakazi wote kwa siku hiyo muhimu Duniani, huku akiweka wazi kuwa Serikali inatambua na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na wafanyakazi wote wa nchini, kazi ambayo ndio msingi wa maendeleo ya Taifa la Tanzania.

"Ninawapongeza sana wafanyakazi wote wa mkoa wa Arusha katika sekta zote, kwa kazi kubwa tunayofanya, kwa maendeleo ya mkoa wetu na taifa kwa ujumla, nawapongeza sana waajiri wote wa Mashirika na Taasisi binafsi, kwa mchango mkubwa wenye tija kwa mkoa na taifa lote kwa ujumla". Amesisistiza Mkuu huyo wa mkoa

Aidha Mheshimiwa Mongela, ameongeza kuwa, usalama wa mkoa wa Arusha, unachangiwa kwa kiasi kikubwa na wafanyakazi, kutokana na watu kuelekeza nguvu, akili na mawazo yote kwenye kufanya kazi, na kuwasisitiza wafanyakazi wote kuendelea kuwa na mshikamano, katika sekta zote, jambo ambalo kimsingi ndilo lenye kuleta tija kwa maendeleo ya Taifa.

Hata hivyo mkuu huyo wa mkoa, amewataka waajiri wote, kuwatambua na kuwapa zawadi stahiki kwa wafanya kazi hodari kila mwaka, jambo ambalo linaongeza motisha kwa wafanyakazi, kuendelea kufanya kazi kwa bidii, pamoja na kupiga marufuku tabia ya baadhi ya waajiri kushindwa kuwatambua wafanyakazihodari, na baadhi kuwatambua na kutokuwapa zawadi zao stahiki.Maadhimisho hayo, yalipambwa na mabango yenye jumbe mbalimbali, ndelemo na vifijo wakati wa maandamano wafanyayakazi hao, pamoja na maonesho ya kazi za taasisi na mashirika mbalimbali zikipita mbele ya mgeni rasmi ndani ya magari.

Awali maadhimisho hayo kwa mwaka 2022, yenye Kauli Mbiu ya "Mishahara na Maslahi Bora kwa Wafanyakazi Ndiyo Kilio Chetu", Kazi iendee, ikionesha namna wafanyakazi wana ari ya kufanya kazi inayokwenda sambamba na mishahara na maslahi bora kwa wafanyakazi wa sekta zote.





Vyumba vitatu vya madarasa Shule ya Sekondari Sokoni II

# TEA YAONDOA MSONGAMANO WA WANAFUNZI MADARASANI SEKONDARI YA SOKONI II

Na Elinipa Lupembe

Katika kuboresha miundo mbinu ya kufundishia na kujifunzia kwenye shule za sekondari za kata, serikali kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania - TEA, imekamilisha ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa, viti na meza 150, shule ya sekondari Sokon II, halmashauri ya Arusha wilaya ya Arumeru.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi shuleni hapo, mkuu wa shule sekondari Sokon II, mwalimu Prisca Mbele, ameweka wazi kuwa, kukamilika kwa vyumba hivyo vya madarasa, kumeondoa msongamano wa wanafunzi darasani na kuwezesha shule hiyo, kufikia malengo ya wastani wa wanafunzi 50 ,kukaa ndani ya chumba kimoja cha darasa, jambo ambalo limefanikisha mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia shuleni hapo.

Aidha Mkuu huyo wa shuke amesema kuwa, ujenzi wa vyumba hivyo 3 vya madarasa umegharama kiasi cha shilingi milioni 60 kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania na kuongeza kuwa, licha ya kuondoa upungufu wa vyumba vya madarasa zaidi umeondoa msongamano wa wanafunzi madarani, na umewezesha shule hiyo kufikia mpango wa uwiano wa wanafunzi 50 kwa darasa moja.

"Tunaishukuru serikali kwa kuweka nguvu kubwa kuboresha miundombinu ya shule yetu, shule haina umri mkubwa tangu ianzihswe mwaka 2015, lakini ina miundombinu inayojjitosheleza, tuna madarasa ya kutosha, shuke ina vyumba 27 vya madarasa , maabara 3 za masomo ya Sayansi, maabara ya somo la ICT, ofisi za walimu, tuna jumla ya wanafunzi 978 wanaotumia wanaotumia vyumba 20 vya madarasa" amefafanua Mkuu huyo wa shule.

Naye mwalimu wa Taaluma shuleni hapo, mwalimu Geofray John amesema kuwa, utoshelevu wa vyumba vya madarasa shuleni hapo, unawezesha walimu kuwafikia wanafunzi wote wakati wa kufundisha, jambo ambalo wanaamini litaimarisha kiwango cha taluma na kupandisha ufaulu shuleni hapo.

Hata hivyo mwalimu huyo wa taaluma, ameweka wazi, kuendelea kuimarika kwa ufaulu shuleni hapo, katika mitihani ya Taifa na kufikia 97.4 % kwa matokeo ya kidato cha nne, na 99.4% kwa matokeo ya kidato cha pili kwa mwaka 2021.

Denning Innocent mwanafunzi wa kidato cha pili, amethibitisha wanafunzi wote kufurahishwa na uwepo wa madarasa ya kutosha shuleni kwao, na kuthibitisha kuwa kunawapa nafasi ya kujifunza katika mazingira mazuri.





Mifugo wakiogeshwa kwenye Josho katika Kijiji cha Lemanda, Kata ya Oldonyosambu

# WAFUGAJI ARUSHA DC WATAKIWA KUTUMIA MAJOSHO KWA UFUGAJI WENYE TIJA

Na Mwandishi wetu

Wafugaji Halmashauri ya Arusha, wametakiwa kutumia majosho, kuogesha mifugo, ili kuwa na mifugo yenye afya bora na yenye tija itakayo waongezea kipato sambamba na kupandisha hali ya uchumi wa familia na Taifa.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mtendaji, halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, wakati akizindua josho la Kanda C, lililofanyiwa ukarabati na wafugaji wa kijiji cha Lemanda kata ya Oldonyosambu, baada ya serikali kuanzisha mkakati wa kutoa dawa za kuogeshea mifugo kwa wafugaji.

Mkurugenzi Msumi, licha ya kuwapongeza wafugaji hao kwa kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya sita, na kuona umuhimu wa kufanya ukarabati wa josho hilo, ili kuikinga mifugo na vifo vinavyotokana na magonjwa yanayoenezwa na wadudu



aina ya kupe na ndorobo, magonjwa ambayo yanauwa mifugo kwa zaidi ya asilimia 70 mpaka 100, na kuwataka wafugaji hao kufanya ufugaji wenye tija kwa kuogesha mifugo pamoja na kuipatia chanjo dhidi ya magonjwa mbalimbali.

"Niwatake wafugaji, kuacha kufuga kwa mazoea, fugeni mifugo michache yenye tija, mifugo ambayo mtaweza kuihudumia kwa kuipa chanjo na kuiogesha, ili mifugo hiyo iweze kuwaingizia kipato, tumieni josho hili, kuogesha mifugo yenu, kama watalamu wa mifugo wanavyowaelekeza".Amesisitiza Mkurugenzi Msumi.

Hata hivyo wafugaji wa kijiji cha Lemanda, wameishukuru Serikali kupitia Wizara ya Mifugo, kwa kuwapatia ruzuku ya dawa ya kuogeshea mifugo, dawa ambayo imewasukuma kukarabati josho hilo, josho ambalo liliacha kutumika zaidi ya miaka 20, kutokana na kushindwa kujiendesha.

Mwenyekiti wa kamati ya kusimamia uendeshaji wa josho la Kanda C, Peter Leskari amesema kuwa, kuzinduliwa kwa josho hilo, kutarudisha matumaini kwa wafugaji ambayo yalipotea kwa muda mrefu, na kusababisha wafugaji kupoteza mifugo na magonjwa yaliyotokana na kupe na ndorobo na kuahidi kusimamia uendeshaji wa josho hilo ili liwanufaishe wafugaji wote wa eneo hilo.

"Josho hili linatupa uhakika kumiliki mifugo yenye afya bora, wafugaji wengi walishindwa kumudu gharama kubwa za kuogesha mifugo nyumbani,na kusababisha mifugo mingi kufa jambo lililozorotesha uchumi wa wafugaji, josho hili, litarudisha matumaini kwa wafugaji" ameweka wazi Mwenyekiti huyo

Naye Afisa Mifugo halmashauri ya Arusha, Omary Sembe, amefafanua kuwa, serikali kupitia wizara ya mifugo, inatekeleza mkakati wa kuboresha sekta ya mifugo na wafugaji, kwa kutoa dawa za kuogeshea mifugo bure.

"Dawa hii inauwezo wa kuikinga mifugo kwa zaidi ya asilimia 70 ya magonjwa yanayotokana na kupe na ndorobo, ikiwemo magonjwa ya ndigana kali, ndigana baridi, moyo kujaa maji, hivyo kuogesha mifugo, kutaondoa vifo vya mifugo visivyo vya lazima" amefafanua Afisa Mifugo.

Awali josho hilo la Kanda C, limekarabatiwa na wafugaji wa kijiji cha Lemanda kwa kushirikiana na halmashauri, kwa gharama ya shilingi milioni 2.8, baada ya serikali kutoa lita elfu 15 za dawa ya kuogeshea mifugo, josho linategemea kuogesha jumla mifugo elfu 90, ng'ombe elfu 15, kondooo elfu 42 na mbuzi elfu 33.





# SERIKALI YAVIKUMBIKA VITUO VYA WALIMU (TRC) ARUSHA DC

Na Elinipa Lupembe

Serikali ya awamu ya sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu, kupitia Wiazara ya Elimu, imevikumbuka vituo vya walimu 'Teacher's Resources Center (TRC)', kwa kuanza kuboresha miundombinu na kuvipa vitendea kazi.

Wizara hiyo ya Elimu, imetoa seti tano za mashine za kudurufia karatasi kwa vituo vitano vya walimu, halmashauri ya Arusha, lengo likiwa ni kuviwezesha vituo hivyo, kuanza kufanya kazi upya, kwa ajili ya kuwaendeleza walimu kitaaluma wawapo kazini.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mashine hizo, Mkurugenzi Mtendaji, halmasahuri ya Arusha, Seleman Msumi, amethibitisha kupokea seti tano za mashine na wino, kutoka Wizara ya Elimu, kwa ajili ya kutumiwa na vituo vitano vya TRC vya halmashauri hiyo.

Mkurugenzi Msumi, amesema Serikali katika kuboresha sekta ya elimu, inajikita pia katika kuboresha mazingira bora kwa kuwapa walimu fursa ya kupata mafunzo kazini, lengo likiwa ni kuwajengea uwezo katika stadi za ujifunzaji na ufundishaji unaoendana na mabadiliko ya kiteknolojia.

"Kazi ya kufundisha inatakiwa kujifunza mara kwa mara, Serikali kupitia vituo vya TRC, imeona umuhimu wa kuvihuisha vituo hivyo, ili walimu waweze kupata mafunzo kazini wakati wote, hivyo niwatake walimu kutumia fursa hiyo adhimu kwa kujinoa kitaaluma pamoja na kubadilishana uzoefu wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, unaoendana na wakati na mabadiliko ya kiteknolojia" amesisitiza Mkurugenzi Msumi

Kaimu Afisa Elimu Msingi, Ruth Sumari, amefafanua kuwa, lengo la serikali kutoa vifaa kwenye vituo vya TRC, ni kuhakikisha walimu wanapata elimu wakiwa kazini, inayowajengea uwezo wa kuendeleza mbinu mbalimbali za ufundishaji ili kuwasaidia wanafunzi kujifunza stadi tatu za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, maarufu kama KK tatu.

Amefafanua kuwa, halmashauri ina jumla ya vituo vitano vya TRC, na kuvitaja vituo hivyo ni pamoja na Kiutu, Mlangarini, Mateves, Oloirien na Lengijave, vituo ambavyo vitahudumia shule zote 132 za serikali za msingi na sekondari za halmashauri.

Hata hivyo, Wasimamizi wa vituo hivyo vya TRC, halmashuri ya Arusha, licha ya kuishukuru na kuipongeza serikali ya awamu ya sita, kwa kuvihuisha vituo vya TRC



, wameweka wazi kuwa vituo hivyo ni muhimu kwa walimu kwa kuwa vinawapa fursa ya kupata mafunzo, mafunzo ambayo yanawezesha walimu kujifunza na kufundisha, kunako endana na wakati, na kuahidi kutumia vituo hivyo kwa maendeleo ya walimu na kupandisha kiwango cha taaluma kwa wanafunzi.



Msimamizi wa TRC Kiutu, na Mratibu wa Elimu kata ya Kiutu, Mwalimu Evaline Mosha, amesema kuwa, TRC ni muhimu sana kwa walimu, kwa kuwa ni kituo kinachowakutanisha walimu kujiendeleza kitaaluma, kwa kujifunza moduli mbalimbali za ualimu zinatolewa na wizara, pamoja na kubadilishana uzoefu katika nyanja za ufundishaji na ujifunzaji wawapo kazini.

Awali halmashauri ya Arusha, inawakaribisha wadau wa maendeleo katika sekta ya elimu, kuendelea kujitoa, kusaidia katika maeneo yote ya halmashauri.





Walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini  Kijiji cha Lemanda,Kata ya Oldonyosambu

# WANUFAIKA WA TASAF III AWAMU YA II, WAMSHUKURU MAMA SAMIA

Na Elinipa Lupembe

Wananchi walioingizwa kwenye mpango wa Mradi wa Kunusuru Kaya Masikini unaotekelezwa na serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF III awamu ya pili, halmashauri ya Arusha, wameshukuru mama Samia na kuipongeza serikali kwa kuwajali na kuwathamini wananchi wasio na uwezo kiuchumi nchini.

Wakizungumza na mwandishi wetu, wakati wa zoezi la kuhawilisha fedha za ruzuku Dirisha la pili  mwaka 2022, wananchi wa kijiji cha Lemanda, wamemshukuru mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu na serikali yake ya awamu ya sita, kwa kuwaingiza kwenye mpango huo, kwa kuwa kijiji hicho hakikuwemo kwenye mpango kwa awamu zilizopita.

"Tunaishukuru serikali kwa kutujali wananchi wa hali ya chini hapa Lemanda, tulikuwa tunakabiliwa na hali ngumu ya maisha, tulikuwa tunaumia sana wenzetu wa vijiji vingine wanapaata hela za TASAF sisi hatupati, lakini sasa tunaahidi kutekelza mashari ya TASAF kwa kanzisha vikundi vya kuweka na kukopa ili tupate mitaji ya kuanzisha biashara ndogo ndogo na tunamuahidi mama hatuamuangusha, tunamuomba Mungu atuwezeshe hela ya mama Samia itupe mafanikiao kwenye familia zetu". Amesisistiza Nshooki Marko.

Naye Upendo Joseph, licha ya kuishukuru serikali amesema kuwa, tangu wameanza kupo mafanikio, kutokana na kuanzisha miradi midogo midogo ya kufuga kuku na kuuza mboga mboga, miradi ambayo imeanza kuwawezesha kuapata fedha ya kujikimu kimaisha.

Diwani wa kata Oldonyosambu, Mhe. Raymond Lairumbe, ameweka wazi kuwa, wananchi wa Oldonyosambu wameridhishwa na kufurahishwa na kitendo cha serikali kuwaingiza, kwenye mpango wa kunusuru kaya masikini mradi unaotekelezwa na TASAF awamu ya IV, na kujioana na wao wamekuwa sawa na wanatanzania wengine, ambao walikuwa wakipokea ruzuku ya fedha kutoka serikalini.

Hata hivyo Mwenyekiti wa Kijiji cha Lemanda, Mosses Kalomba, amefafanua kuwa, wao kama viongozi wataendelea kuwasimamia wanufaika hao wa TASAF, kutumia fedha hizo vizuri kwa kufanya biashara ndogo ndogo ili kuinua uchumi na pato la familia, na kuongeza kuwa tayari wamewahamasisha wanufaika hao, kujiunga na BIMA ya Afya iliyoboreshwa ili weweze kuwa na uhakika wa kupata matibabu pindi wanapougua.

Naye Mkurugenzi Mtendaji, halmashauri ya Arusha Seleman Msumi, amewataka wanufaika hao wa TASAF, kutumia  vizuri fedha wanazopokea kwa kufanya biashara na kuanzisha miradi midogo midogo katika maeneo yao, ili kujikwamua katika hali ya umasikini uliokuwepo.

"Tujitahidi kutumia fedha tunazopewa na serikali vizuri ili kujikwamua na hii ya umasikini pamoja na kuhakikisha tunaboresha hali zetu za kimaisha" amesisitiza Mkurugenzi Msumi.

Hata hivyo Mratibu wa TASAF, Halmashauri ya Arusha, Grace Makema, amesema kuwa jumla ya shilingi bilioni 1.178, zimetolewa na kuhawilishwa kama ruzuku kwa jumla ya kaya 14,135  kwenye vijiji 88 vya halmashauri ya Arusha kwa awamu mbili za mwezi Novemba na Desemba na Januari na Februari 2022.



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# HALMASHAURI YA WILAYA ARUSHA

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

## EWE MWANANCHI KUMBUKA KUSHIRIKI VYEMA ZOEZI LA SENSA NA MAKAZI YA 2022

### UMUHIMU WA SENSA YA WATU NA MAKAZI MWAKA 2022

1. Kuisaidia serikali kupata taarifa za za msingi zitakazosaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya maendeleo ya mwaka 2025, mageuzi ya masuala ya afya na jamii, pamoja na ufuatiliaji wa ajenda za maendeleo za kimataifa.
2. Taarifa za idadi ya watu husaidia katika mamlaka za wilaya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huaksi matakwa ya watu katika ngazi husika na kusaidia uwiano wa mgawanyo wa rasilimali.
3. Taarifa za msingi za hali ya kidemografia, kijamii na kiuchumi za idadi ya watu na makazi za mipango katika ngazi zote
4. Kigawio katika kukokotoa viashiria vingine mfano pato la mtu mmoja mmoja, pato la Taifa, Ajira na ukosefu wa Ajira na kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi.
5. Taarifa itakayowezesha Serikali kujua ongezeko la watu, kwa mgawanyo na viashiria vingine ambavyo ni muhimu kwa usimamizi wa mazingira.
6. Msingi wa utawala bora na ujumuishaji wa Demokrasia. Takwimu sahihi za sensa zinahitajika kwa ajili ya ugawaji wa majimbo ya uchaguzi kwa ufanisi, kurekebisha mipaka ya kiutawala katika serikali za mitaa.

**"ARUSHA DC TUPO TAYARI KUSHIRIKI SENSA YA WATU NA MAKAZI"**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
**HALMASHAURI YA WILAYA ARUSHA**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

# ARUSHA DC TUPO TAYARI KUHESABIWA
# WEWE JE?

KUHESABIWA NDO MPANGO MZIMA

www.arushadc.go.tz


#kazi inaendelea


HALMASHAURI YA ARUSHA
WILAYA YA ARUMERU
TANZANIA
SENSA
23 Agosti
2022
Jiandae Kuhesabiwa
SENSA
YA WATU NA MAKAZI
NI NINI?
Ni zoezi Muhimu linalokusanya Taarifa za kila Mtu aliyelala ndani ya Mipaka ya Halmashauri usiku wa kuamkia siku ya Sensa.
SELEMAN MSUMI
DED ARUSHA DC
www.arushadc.go.tz
arusha_district_council
Arusha District Council


HALMASHAURI YA ARUSHA
WILAYA YA ARUMERU
TANZANIA
SENSA
23 Agosti
2022
Jiandae Kuhesabiwa
Taarifa zote utakazotoa kwa Karani wa Sensa ni SIRI na zitatumika kwa madhumuni ya Kitakwimu pekee.
SISI TUKO TAYARI
KUHESABIWA!
WATUMISHI WA HALMASHAURI YA ARUSHA
www.arushadc.go.tz
Arusha District Council
arusha_district_council


TANZANIA
SENSA
2022
MIMI
NITAONYESHA USHIRIKIANO KATIKA ZOEZI LA SENSA
WEWE JE?
Watu wote watakaolala katika Kaya binafsi usiku wa kuamkia Siku ya Sensa pamoja na Watu wote watakaokuwa katika Kaya za Jumuiya watahesabiwa kwa utaratibu Maalumu.
MHE. OJUNG'U SALEKWA


HALMASHAURI YA ARUSHA
Kuripoti
Kazini Kwa
Waajiriwa
Wapya Kada ya
Elimu na Afya
"Ninawakaribisha Watumishi wote waliopangiwa kufanya kazi katika Halmashauri ya Arusha Wilaya ya Arumeru" DED ARUSHA DC
KARIBUNI SANA
Kwa Maelezo au Msaada wasiliana nasi Kwa Namba zifuatazo:-
MAWASILIANO
MKurugenzi Mtendaji (W) +255 787 559 025
Afisa Utumishi (W) +255 758 206 663
Afisa Elimu Msingi (W) +255 715 369 160
Afisa Elimu Sekondari (W) +255 762 630 723
Mganga Mkuu (W) +255 754 761 775
Katibu wa Afya +255 755 777 194
www.arushadc.go.tz
Arusha District Council


HALMASHAURI YA ARUSHA
WILAYA YA ARUMERU
SENSA
2022
SISI WANAFUNZI WA
Shule ya SEKONDARI ILKIDING'A
TUKO
TAYARI
KUHESABIWA


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA ARUSHA
Siku ya Mtoto wa Afrika 2022
SISI WOTOTO WA ARUSHA DC
TUKO TAYARI KUHESABIWA
WEWE JE?
SENSA
2022


HALMASHAURI YA ARUSHA
WILAYA YA ARUMERU
SENSA
23 Agosti
2022
Jiandae Kuhesabiwa
MIMI
NIKO TAYARI
KUHESABIWA.
WEWE JE?
Shiriki Kikamilifu Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 kwa Maendeleo Endelevu ya Taifa letu
SELEMAN MSUMI
DED ARUSHA DC
www.arushadc.go.tz
Arusha District Council
arusha_district_council




# FAHARI YETU
## HALMASHAURI YA ARUSHA

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

enaboishu
FM RADIO 101.3

**Imetolewa na;**
**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Halmashauri ya Arusha**

**Mhariri Mkuu**
Seleman H. Msumi
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Arusha

**Mhariri Msaidizi**
Elinipa J. Lupembe
Afisa Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Arusha

Msanifu
**Daniel Zacharia**

Mawasiliano
**S.L.P 2330, Arusha**
**baruapepe:ded@arushadc.go.tz**

www.arushadc.go.tz
Arusha District Council
arusha_district_council